JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA SINGIDA

TAARIFA FUPI KUHUSU HALI YA HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

JUNI, 2017.

Imeandaliwa na: Julai, 2017

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,

Sehemu ya Huduma za Maji,

S.L.P 5,

SINGIDA.

1.0 Utangulizi

Huduma ya maji vijijini inayotolewa kwa sasa inawafikia asilimia **44** ya Wananchi. Baadhi ya miradi ya maji vijijini haifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchakavu. Juhudi za kuifanyia miradi hiyo matengenezo na ukarabati zinaendelea kwa kutumia fedha kutokana na vyanzo mbalimbali hasa Programu ya Kitaifa ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II).

2.0 Hali ya Huduma ya Maji Vijijini

Hadi kufikia mwezi Juni, 2017 asilimia **44** ya wakazi waishio vijijini katika Mkoa wa Singida wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia miradi ya maji iliyopo. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika kila halmashauri ya Wilaya kwa maeneo ya vijijini ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1a**. Wananchi wengi waishio vijijini hutegemea zaidi vyanzo vya maji ya visima ambavyo kwa Mkoa wa Singida kuna jumla ya visima virefu **250**, visima vya kati **267** na visima vifupi **620** ambavyo vinatumika kama vyanzo vya maji kwa jamii ya Singida. Aidha kuna Malambo **109** na Mabwawa **9** kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.1b.** ambayo hutumika kwa kunyeshea mifugo na shughuli zingine za uzalishaji hata hivyo malambo na mabwawa hukauka kipindi cha kiangazi na kusababisha hali duni ya upatikanaji wa maji.

Jedwali Na. 1a: Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini katika kila Halmashauri ya Wilaya

Na.	Halmashauri	Idadi ya Watu Vijijini	Idadi ya Watu Wanaopata maji vijijini	Idadi ya Vituo vya kuchotea maji	Asilimia ya watu wanaopata huduma ya Maji
1	Singida MC	84,857	41,580	251	53
2	Singida DC	246,996	130,908	689	44
3	Manyoni DC	213,010	41,803	488	55
4	Mkalama DC	208,772	89,772	468	43
5	Itigi DC	112,565	34,896	89	42
6	Ikungi DC	309,321	99,234	282	32
7	Iramba DC	261,368	120,200	753	32
	JUMLA	**1,371,741**	**600,881**	**3,020**	**44**

Jedwali Na. 1b: Vyanzo vya Maji Vijijini katika kila Halmashauri ya Wilaya

Na.	Halmashauri	Idadi ya visima virefu	Idadi ya visima vya kati	Idadi ya visima vifupi	Idadi ya malambo	Idadi ya mabwawa
1	Singida MC	32	5	32	0	0
2	Singida DC	31	41	192	17	1
3	Manyoni DC	19	9	16	14	2
4	Mkalama DC	108	0	76	20	0
5	Itigi DC	19	19	1	6	3
6	Ikungi DC	11	76	248	22	3
7	Iramba DC	30	117	55	30	0
	JUMLA	**250**	**267**	**629**	**109**	**9**

3.0 Mpango wa Kuongeza Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini

(a) Miradi Inayoleta Matokeo ya Haraka

Katika hatua za awali za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, utekelezaji ulianza na miradi midogo midogo inayoleta matokeo ya haraka. Miradi hiyo ilitekelezwa katika miaka ya 2007/2008 na 2008/2009. Fedha za kutekeleza miradi hiyo zilisitishwa kutolewa mwezi Juni, 2009 ili kuanza kutekeleza miradi mikubwa ya vijiji 10 katika kila Halmashauri.

(b) Utekelezaji wa Miradi katika Vijiji 10 katika kila Halmashauri

Vijiji vilivyopewa kipaumbele katika kupata huduma ya maji kupitia Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa Programu chini ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika Halmashauri za Mkoa wa Singida vimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

Jedwali Na. 2: Vijiji Vilivyopewa Kipaumbele na Halmashauri katika kutekeleza

HALMASHAURI	VIJIJI VILIVYOPEWA KIPAUMBELE
Singida DC	Mjughuda, Ughandi 'A', Laghanida, Mipilo, Sefunga na Itaja
Singida MC	Kisaki, Unyianga, Mtamaa-A, Mtamaa-B, Mwankoko-A, Mwankoko-B, Ititi, Uhamaka, Manga na Mtipa,
Itigi DC	Doroto,Itigi mjini,Mwamagembe na Rungwa
Ikungi DC	Puma, Siuyu, Nkhoiree, Nkuhi na Mgungira.
Iramba DC	Nguvumali,Nga'nguli,Mingela,Mgungia,Mlandala na Ujungu
Manyoni DC	Londoni, Nkonko, Majiri, Iseke, Saranda, Muhalala, Solya/Kilimatinde, Mpola,
Mkalama DC	Iguguno, Kikhonda, Kidarafa, Muntamba, Gumanga, Mkalmaa na Nyahaa

c) Ujenzi wa Miundombinu ya Maji

Hadi kufikia mwezi Juni, 2017 jumla ya miradi **48** katika Halmashauri za Mkoa wa Singida ilipangwa kujengwa, miradi **05** ilikuwa inaendelea na ujenzi ambapo miradi **43** ujenzi wake umekamilika na inatoa huduma ya maji kwa wananchi kama ambavyo inaonekana katika **Jedwali Na. 3.**

Jedwali Na. 3: Miradi iliyopangwa kutekelezwa na inayotekelezwa

Maelezo ya Miradi ya BRN iliyopendekezwa	Miradi iliyopangwa kutekelezwa hadi kufikia Juni, 2016/2017							
	Itigi DC	**Ikungi DC**	**Iramba DC**	**Mkalama DC**	**Manyoni DC**	**Singida DC**	**Singida MC**	**Jumla ya Miradi**
Miradi ya Maji ya Vijiji 10 (WSDP)	1	3	6	7	3	5	10	**35**
Miradi ya Ukarabati na/au upanuzi	2	1	0	0	6	0	0	**09**
Miradi ya Quickwin	0	3	0	0	0	1	0	**04**
Miradi ya Kitaifa	0	0	0	0	0	0	0	**00**
JUMLA	**3**	**7**	**6**	**7**	**9**	**6**	**10**	**48**

Aidha, Utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu katika miradi ya maji Vijiji 10 vilivyoainishwa na Halmashauri husika kulingana na fedha iliyotengwa umefanykia kama ifuatavyo:

i) Singida DC: Vijiji 5 kati ya 6 vimekamilika na Wananchi wanapata huduma katika vijiji 4 kati ya 6 (kijiji cha Sefunga kisima kilikauka na Pohama ujenzi unaendelea)
ii) Singida MC: vijiji **10** kati ya **10** vimekamilika na Huduma imeanza kutolewa
iii) Mkalama DC: Vijiji 5 kati ya 7 vimekamilika na Huduma imeanza kutolewa
iv) Itigi DC: Vijiji **3** kati ya **3** vimekamilika na Wananchi wanapata huduma.Miradi mipya 5 imeanza kutekelezwa kupitia awamu ya pili ya Programu ya maendeleo ya Sekta ya maji.
v) Iramba DC: Vijiji 3 kati ya 6 vimekamilika na Wanachi wanapata huduma
vi) Ikungi DC : Vijiji 5 kati ya 7 Vimekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji. Miradi mipya 3 imeanza kutekelezwa kupitia awamu ya pili ya Programu ya maendeleo ya Sekta ya maji.
vii) Manyoni DC : Vijiji **9** kati ya **9** vimekamilika na Wananchi wanapata huduma

Jedwali Na. 4 linaonyesha hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Halmashauri.

Jedwali Na. 4: Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji

Halmashauri	Vijiji vinavyotekelezwa	Hatua iliyofikiwa ya utekelezaji
Singida DC	Ughandi 'A', Laghanida, Mipilo, Sefunga, Mjughuda na Pohama	- Upanuzi wa miundombinu ya maji katika kijiji cha Pohama umefikia asilimia 85% - Kijiji cha Sefunga kisima kilikauka.
Singida MC	Kisaki, Unyianga, Mtamaa-A, Mtamaa-B, Mwankoko-A, Mwankoko-B, Itiiti, Uhamaka, Manga na Mtipa,	- Miradi yote ya awamu ya kwanza WSDP I imekamilika asilimia 100% na imeanza kutoa huduma kwa jamii. - Mradi wa maji wa kijiji cha Mwankoko-B umekabidhiwa kwa Mamlaka ya maji Singida (SUWASA) Kwa ajii ya uendeshaji.
Itigi DC	Ipande, Sanjaranda, Idodyandole, Mitundu, Kintamula, Rungwa, Doroto na Mwamagembe	Ipande (60%), Sanjaranda (55%),Idodyandole,Mitundu, na Kintanula (78%) Miradi ya vijiji vya Rungwa, Doroto na mwamagembe imekamilika na inatoa huduma ya maji
Iramba DC	Mgungia,Mlandala, Ujungu, Nguvumali, , Ng'ang'uli, na Mingela.	-Mradi wa maji kijiji cha Mgungia umefikia hatua ya asilimia 87%, utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya maji inaendelea. - Mradi wa maji kijiji cha Mlandala umefikia hatua yaasilimia 95%, utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya maji inaendelea - Mradi wa maji kijiji cha Ujungu umefikia hatua yaasilimia 86%, utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya maji inaendelea. -Mradi wa maji katika vijiji vya Nguvumali, Ng'ang'uli na mingela inafanya kazi.
Mkalama DC	Gumanga, Muntamba, Nyahaa, Mkalama, Kidarafa, Kikhonda na Iguguno.	-Upanuzi wa mradi wa maji Gumanga umefikia asilimia 45 huku mradi wa maji Muntamba umefikia asilimia 95. -Ujenzi wa miundombinu ya maji Nyahaa umefikia aslimia 80. -Miradi ya maji katika vijiji vya Mkalama, Kidarafa, Kikhonda na Iguguno inafanya kazi.
Ikungi DC	Musimi, Iyumbu, Ntewa, Muhintiri, na Mkiwa. Siuyu, Puma, Nkuhi, Mgungira, Nkhoiree	- Ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji ya vijiji vya Mgungira, Nkhoiree, Nkuhi, Puma, Siuyu, Musimi na Iyumbu imekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji. - Ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji ya vijiji vitatu unaendelea kama ifuatavyo Ntewa (73%), Muhintiri (42%) na Mkiwa (68%).
Manyoni DC	Londoni, Nkonko, Majiri, Iseke, Saranda, Muhalala, Solya/kilimatinde, Mpola,	- Miradi yote ya awamu ya kwanza WSDP I imekamilika asilimia 100% na imeanza kutoa huduma kwa jamii. - Mradi wa Saranda ulifadhiliwa na World vision.

4.0 Fedha za Utekelezaji wa Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa Mwaka 2016/2017

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, kiasi cha **Shilingi 4,020,890,142** kilitengwa kwenye bajeti za Halmashauri za Mkoa wa Singida. Mchanganuo wa kiasi cha fedha zilizotengwa kwenye Halmashauri kimeonyeshwa katika **Jedwali Na. 6**. Hadi kufikia Mwezi Juni 2017, Wizara imetuma jumla ya **Shilingi 2,802,338,665.00** kwenda Halmashauri za Mkoa wa Singida kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7**

Jedwali Na. 6: Fedha zilizotengwa katika bajeti kwa Mkoa wa Singida kwa Mwaka 2016/17

Mkoa	Halmashauri		Bajeti Fedha za Ndani (Sh)	Bajeti Fedha za Nje (Sh)	Jumla ya Bajeti (Sh)
Singida	Ikungi	DC	490,415,101	166,757,940	657,173,041
	Iramba	DC	387,517,030	168,890,129	556,407,159
	Manyoni	DC	380,000,000	135,567,982	515,567,982
	Mkalama	DC	520,751,364	115,599,926	636,351,289
	Singida	DC	491,909,375	66,974,923	558,884,298
	Singida	MC	875,064,778	221,441,594	1,096,506,372
Jumla	**Shilingi**		**3,145,657,648**	**875,232,494**	**4,020,890,142**

***** *Halmashairi ya wilaya ya Itigi ilianzishwa baada ya bajeti kupitishwa.*

Jedwali Na. 7: Fedha Zilizotolewa kwa Mwaka 2016/2017 hadi 30 Juni, 2017

Mkoa	Halmashauri	Fedha zilizotolewa (Tshs)**
Singida	Itigi DC	1,102,634,255
	Manyoni DC	46,653,000
	Iramba DC	529,496,328
	Ikungi DC	293,494,278.46
	Singida DC	374,217,804
	Singida MC	30,000,000
	Mkalama DC	425,843,000
	Jumla (Tshs)	**2,802,338,665**

Jedwali Na. 8: Fedha zilizotengwa katika bajeti kwa Mkoa wa Singida kwa Mwaka 2017/18

Na	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani			Fedha za Nje			Jumla
			Ujenzi wa Miundombinu ya Maji	Usanifu, Usimamizi na Ufuatiliaji.	Uendeshaji wa Ofisi na Mateng enezo.	Ujenzi wa Miundombinu ya Maji.	Payment by Results (PbR)	Kampeni ya Kitaifa Usafi wa Mazingira	
1	Ikungi	DC	401,167,000	40,000,000	12,000,000	46,833,000	152,296,000	31,000,000	683,296,000
2	Iramba	DC	527,043,000	40,000,000	12,000,000	59,842,000	156,440,000	41,000,000	836,325,000
3	Itigi	DC	401,167,000	40,000,000	12,000,000	46,833,000	20,203,000	26,000,000	546,203,000
4	Manyoni	DC	401,167,000	40,000,000	12,000,000	46,833,000	80,810,000	31,000,000	611,810,000
5	Mkalama	DC	401,167,000	40,000,000	12,000,000	46,833,000	104,121,000	26,000,000	630,121,000
6	Singida	DC	401,167,000	40,000,000	12,000,000	46,833,000	334,119,000	26,000,000	860,119,000
7	Singida	MC	413,167,000	30,000,000	10,000,000	46,833,000	65,788,000	21,000,000	586,788,000

1. Changamoto za Sekta ya Maji

Mkoa wa Singida unakabiliana na changamoto zifuatazo katika utoaji wa huduma za maji;-

(a) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya ujenzi, ukarabati, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maji.

(b) Kiasi kikubwa cha chumvi kwenye maji, japo yanakidhi viwango vya ubora lakini ladha inakuwa kero na kupelekea wananchi kuyakwepa kwa kunywa, pia kusababisha uharibifu wa vifaa tiba.

(c) Upungufu wa fedha za usimamizi wa miradi kwa ajili ya RWST na CWSTs na fedha za uendeshaji na matengenezo ya magari;

(d) Uhaba wa wataalam, upungufu wa magari na vyombo vingine vya usafiri

(e) Upungufu mkubwa wa fedha za matumizi ya kawaida (OC) hali ambayo imepelekea halmashauri zote kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

(f) Kutokuwapo kwa vitendea kazi hasa magari kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi. Halmashauri 2 kati ya 7 ndizo zenye magari na pikipiki zilizopo ni 9 ambapo 5 ni nzima na 4 ni mbovu.

(g) Kutokuwa na wataalamu wa kutosha hasa wahandisi na mafundi sanifu kwa ajili ya usanifu, usimamizi na uendeshaji wa miradi, kwa sasa kuna Wahandisi 12 kati ya 25 wanaohitajika.

(h) Deni kubwa la Ankara za nyuma za nishati ya umeme kwa ajili ya uzalishaji wa Maji kwa wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira (SUWASA) ya makao makuu ya

Mkoa ambapo hadi sasa Mamlaka inadaiwa kiasi cha Milioni 510, hali inayosababishiwa kusitishiwa huduma ya Umeme mara kwa mara.

(i) Kutokuwepo kwa mtandao wa maji taka kuna athiri usafi wa mazingira, mradi wa utoaji wa maji taka Mjini Singida umeshafanyiwa usanifu na unasubiri kiasi cha dola za kimerekani US$ 47,256,599.60 ili kuanza ujenzi wa mradi

(j) Ukosefu wa vitendea kazi muhimu kwa mamlaka ya SUWASA kama Excavator, Mtambo wa kanyanyua mizigo "crane" ya kuanzia tani 10 kwa kazi za matengenezo makubwa ya visima na mabomba makubwa

(k) Ucheleweshwaji wa fedha za utekelezaji na usimamizi wa miradi.

2. Mikakati ya uboreshaji wa Huduma za maji Mkoani

(a) Kufanya utafiti wa vyanzo vipya vya maji na kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua.

(b) Kushirikiana na Wizara ya Maji kuendelea kutafuta wafadhili kugharamia gharama za ujenzi za mradi wa mtandao wa Maji taka kwa Singida Mjini, na Mradi wa Maji safi kwa miji midogo ya Kiomboi na Manyoni

(c) Kuangalia uwezekano wa kushirikisha taasisi za dini na sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya maji – kuongeza kasi ya Serikali katika kukabiliana na uhaba mkubwa wa huduma za maji uliopo hususani maeneo ya vijijini.

(d) Serikali ya Mkoa tayari imechukua hatua ya kuweka ulinganifu/ usawa wa rasilimali watu kwa kuwahamisha kutoka maeneo yenye unafuu kwenda penye upungufu mkubwa zaidi ndani ya Mkoa na kuendelea kuomba vibali vya kuajiri watumishi wapya toka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

(e) Serikali kujipanga kulipa madeni makubwa ya taasisi zake inayodaiwa na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kwa kuingiza madeni hayo kwenye bajeti.

(f) Kufunga dira za malipo ya kabla kwenye taasisi zenye madeni ili kuzuia ongezeko la madeni hayo

(g) SUWASA inaandaa andiko la mkopo wa **Tshs.750,000,000** ili kuongeza mtandao zaidi ya kilometa 15 kwenye maeneo yasiyo na mtandao wa mabomba.

3. Kero za Sekta ya Maji

(a) Uhaba wa huduma ya maji – hadi sasa ni pungufu ya nusu ya wakazi wa Mkoa huu waishio Vijijini ndio wanaopata maji safi na salama.

(b) Ucheleweshaji wa fedha za malipo ya miradi iliyokwishaanza jambo linalopelekea kuchelewa kukamilika kwa miradi husika na wananchi kukosa huduma kwa muda mrefu.

4. Hatua na mikakati itakayochukuliwa na Mkoa katika kutatua kero hizo

Mkoa unapanga kushirikisha wadau zaidi ili kuwezesha upatikanaji wa uwekezaji utakaoongeza kasi ya ujenzi wa miradi ya Maji. Wadau wafuatao wameainishwa:-

(a) Taasisi za Dini

(b) Sekta binafsi

(c) Mashirika yasiyo ya Kiserikali